# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 19 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Septemba 2023

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

# Rais Samia ataka unafuu mbolea ya ruzuku



**Muktasari:**

Rais Samia aagiza viongozi wa Wizara za Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha, kukaa pamoja ili kuangalia gharama za kupelekea mbolea ya ruzuku kwa bei nafuu kwa wakulima wa maeneo mbalimbali.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan (katikati) akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (hayupo pichani) alipotembelea banda la Mamlaka wakati wa kilele cha maonesho na sherehe za wakulima (nanenane) zilizofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya Tarehe 08.08.2023.

## TOLEO MAALUM USHIRIKI WA TFRA MAONESHO YA NANENANE 2023

NDANI>>

BANDA LA TFRA LAWAVUTIA VIONGOZI WENGI 5



TFRA ILIVYOJIZOLEA TUZO KWA UTENDAJI ULIOTUKUKA 10

WAKULIMA WA MAKAMBAKO WANUFAIKA NA ELIMU YA MBOLEA NANENANE 14

# Rais Samia ataka unafuu mbolea ya ruzuku

Rais Samia Suluhu Hassan amemwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kukaa na Wizara ya Fedha ili kuangalia gharama za usambazaji wa mbolea ya ruzuku kwa lengo la kuleta unafuu kwa wakulima.

Rais Samia alitoa agizo hilo, tarehe 8 Agosti, 2023 wakati wa kilele cha maonyesho ya wakulima, Nanenane yaliyofanyika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.

Maonyesho ya mwaka huu, yalibeba kauli mbiu ya 'vijana na wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu ya chakula'. Ambapo Rais Samia alisema kauli mbiu hiyo inalenga kutambua mchango wa vijana na wanawake katika kilimo, mifugo na uvuvi.

Rais Samia alisema moja ya changamoto iliyojitokeza msimu uliopita wa kilimo ni kuifikisha mbolea ngazi ya kata, akisema bei ya mfumo ilikuwa Sh 70,000 kwa mfuko mmoja.

"Sasa mara hii ni Sh 85,000 pamoja na gharama ya kufikisha mbolea kwa wakulima, nikuagize waziri (Bashe) angalieni namna ya kupata gharama za usambazaji angalau kwa mawakala wakubwa ili kuleta ahueni kwa wananchi angalau Sh5, 000 itolewe.

"Serikali ichangie na mkulima achangie ili mbolea ifike, tumsipe mzigo mkubwa sana mkulima, naomba mkazitazame bei za mbolea," alisema.

Alisisitiza kuwa, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea ili kuongeza uzalishaji wa mazao, huku akiwaomba wakulima kuendelea kujisajili na kuhakiki taarifa zao za usajili ili kuwezesha kununua mbolea hiyo.

Katika hatua nyingine, Rais Samia alisema ajenda ya Serikali ni kuongeza mchango wa sekta ya kilimo hadi asilimia 10, kufikia mwaka 2030 akisema uwezekano huo upo.

Alisema ndio maana Serikali inaelekeza nguvu kubwa katika sekta ya kilimo, ambapo pia masuala ya uvuvi na ufugaji yamepewa umuhimu mkubwa.

Katika kufanikisha hilo, Rais Samia alisema Serikali imechukua hatua kadhaa katika kuelekeza nguvu ikiwemo kuongeza bajeti za sekta husika ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Lengo la Serikali ni kutumia hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ambapo kwa sasa zaidi ya hekta 700,000 ndizo zinazotumika katika umwagiliaji na milioni 28 zimebaki," alisema.

Mbali na hilo, aliwataka maofisa ugani kukaa katika maeneo waliyopangiwa ili kuwasaidia wakulima na wafugaji kwa kuwapatia utalaamu na mbinu za kisasa za uzalishaji.

Pia alikubaliana na ombi la mbunge wa Mbeya Mjini aliyeomba muda wa maonyesho hayo kuongezwa kwa siku saba ili kutoa fursa kwa wananchi kufanya biashara zao hadi pale Mamlaka zitakapoanza mchakato wa kuboresha viwanja hivyo.

"Naungana na Spika (Dk Tulia) kutoa wiki moja zaidi kwa wawekezaji hasa wale waliotoka nyanda za juu kusini ili kuendelea kuonyesha na kuchukua vifaa. Nimwagize Bashe aongeze siku nyingine saba," alisema.




Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (mwenye mic) akizungumza mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) alipotembelea banda la Mamlaka wakati wa kilele cha maonesho na sherehe za wakulima (nanenane) zilizofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya Tarehe 08.08.2023.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan (mwenye gauni la kijani) akikaribishwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe katika banda la Kijiji cha mbolea lililojumuisha wafanyabiashara na wazalishaji wa mbolea ndani ya viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya ikiwa ni miongoni mwa mabanda yaliyotembelewa na Mhe. Rais wakati wa kilele cha maonesho na sherehe za wakulima (nanenane).



# Makamu wa Rais Dkt. Mpango aitaka TFRA kufikisha mbolea karibu na wakulima

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuhakikisha mbolea inafikishwa karibu na wakulima ili kuwaondolea usumbufu na gharama ya kufuata mbolea mbali na wanakolima.

Pamoja na kuikisha mbolea hiyo, Dkt. Mpango alisema mbolea hiyo ifike kwa wakati ili msimu wa kupanda ukifika wakulima waweze kuitumia mbolea hizo kulingana na mahitaji yao.

Dkt Mpango alitoa kauli hiyo tarehe Mosi Agosti, 2023 alipotembelea banda la Mamlaka lililokuwepo ndani ya viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.

Aidha, Dkt. Mpango ameitaka TFRA Kuendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wafanyabiashara wanaochakachua mbolea pili liwe fnzo kwa wengine na hatimaye kukomesha kabisa tabia hiyo miongoni mwa wafanyabiashara.

Akieleza mpango wa Serikali kwa msimu wa kilimo 2023/2024 Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo alisema ili kuondoa adha ya wakulima kufuata mbolea maeneo ya mbali vyama vya ushirika vitatumika ili kuuza mbolea kwa wakulima.

Alisema, kwa sasa serikali imetoa bei elekezi za mbolea mpaka Kijiji cha mwisho kabisa ili pia kuwapa nguvu ya kufikisha mbolea katika maeneo ya pembezoni mawakala na wafanyabiashara kutokana na bei elekezi kufidia kwenye gharama ya usafiri.

Aidha, Dkt. Ngailo alikiri kupokea maelekezo na kueleza kuwa Mamlaka itafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na Serikali kwa ajili ya kuhakikisha wakulima wananufaika na mbolea za ruzuku zinazotolewa na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.





Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Isdory Mpango akiwa katika banda la TFRA leo katika viwanja vya Nanenane- John Mwakangale jijini Mbeya ambapo aliielekeza Mamlaka kuhakikisha kuwa mbolea zinafika kwa wakati kwa wakulima ili kuondoa malalamiko na kushughulikia kesi za uchakachuaji wa mbolea nchini.

# Banda la TFRA lawavutia viongozi wengi

Unawezaje kuyaelezea kwa ufupi Maonesho ya 2023 ya Nanenane kitaifa na kimataifa? Pengine hili ni swali gumu kulijibu kwa urahisi kwa sababu linategemea vionjo na mtazamo wa mtu binafsi. Lakini ukweli uliodhihiri ni kwamba kwa Watanzania waliohudhuria maonesho hayo kwenye kanda zote na kujionea kile kilichotendeka katika mabanda mbalimbali ili kuimarisha sekta ya kilimo nchini, Nanenane ya mwaka huu ilitia fora na kuwa kivutio kwa watu wa kila tabaka katika jamii yetu.

Ni maonesho yaliyowavuta viongozi mbalimbali wa kitaifa, watunga sera, wataalam wa kilimo, wakulima kutoka sehemu mbalimbali nchini na nje ya nchi. Kwa miaka mingi, Tanzania imekuwa kivutio kutokana na nafasi yake kijiografia na fursa lukuki za uwekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi katika eneo hili la Afrika Mashariki na Kati.

Katika maonesho ya kitaifa na kimataifa yaliyofanyika kwa siku nane kuanzia Agosti 1 hadi 8 katika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya, watu waliofurika katika uwanja huo walishuhudia kuundwa kwa Kijiji cha Mbolea ambapo Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) ilishirikiana na kampuni za mbolea, wazalishaji na waingizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi ili kuhamasisha umma kutembelea na kupata elimu kuhusu masuala ya mbolea nchini.

Kampuni au taasisi zilizounda Kijiji cha Mbolea ni pamoja na Mradi wa TAISP ulio chini ya Wizara ya Kilimo unaoshughulikia masuala ya ruzuku ya pembejeo za kilimo ikiwa ni mbolea na mbegu, Kampuni ya Mbolea (TFC), Kampuni ya Mbolea ya ITRACOM, Kampuni la Uchimbaji Madini na Mbolea ya Minjingu (MMFL), Kampuni ya Guavay (Hakika), Kampuni ya YARA (T) Ltd.,Kampuni ya OCP (T) Ltd., Kampuni ya ETG Inputs Ltd., Kampuni ya Mwana wa Africa, Kampuni ya Premium Agrochem Ltd., na Kampuni ya One Acre Fund.

Kijiji hiki cha Mbolea kilikuwa ni sumaku iliyowavuta wageni wa tabaka zote katika jamii, kuanzia Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango, viongozi wa mikoa na wilaya na maelfu ya wananchi wa kawaida waliovutwa kujionea yale yanayotendeka katika tasnia ya mbolea ili kukuza sekta ya kilimo kwa ujumla wake.

Banda la TFRA lilimvuta Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiongozwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Mohamed Bashe.

Katika banda hilo Rais alipokea shukrani kwa kusimama kidete katika kuhakikisha mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 unatekelezeka na kuelezwa kuhusu mikakati ya utekelezaji wa mpango huo kwa msimu wa kilimo 2023/2024.

Pamoja na fursa ya kutembela banda hilo na kupata mafunzo jinsi TFRA inavyotekeleza shughuli zake, Rais aliitaka taasisi hiyo ya serikali kufanya tahmini ya matokeo ya ruzuku ya mbolea iliyotolewa kwa wakulima kupitia ongezeko la uzalishaji kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023.

Waziri wa Kilimo alimshukuru Rais kwa kutoa fedha zilizowezesha ruzuku ya mbolea kwa wakulima msimu 2022/2023 na kukubali kutenga fedha tena kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima msimu 2023/2024.

Naye Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango, alipotembelea banda la TFRA wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya Nanenane 2023 Kitaifa na Kimataifa pamoja na kujifunza masuala kadhaa kuhusu shughuli za taasisi hiyo alitoa maagizo kadhaa; mojawapo aliitaka TFRA kuhakikisha mbolea inafika karibu na wakulima, bidhaa hiyo inapatikana kwa wakati kwa wakulima na kuendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wafanyabiashara waovu wanaochakachua mbolea.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, alifurahishwa na kazi nzuri inayofanywa na TFRA na kuitaka taasisi hiyo iwezeshe kushamiri kwa biashara ya mbolea kwa kuwatia moyo wafanyabiashara na wadau wengine waifurahie shughuli hiyo badala ya kujikita kwenye udhibiti peke yake.

Kwa ujumla, viongozi mbalimbali wa kitaifa waliotembelea mabanda ya TFRA katika viwanja mbalimbali vya kanda nchini walipongeza kusikia namna Mamlaka ilivyojipanga kusimamia upatikanaji na usambazaji wa mbolea wenye lengo la kuwahamasisha wakulima kuongeza tija kwenye kilimo, hasa kutokana na azma ya taifa ya kujitosheleza kwa chakula kwa miongo ijayo ikikumbukwa Tanzania inashuhudia kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu.

Pamoja na mambo mengine viongozi hao waliiomba serikali kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima na kusimamia ubora wa pembejeo hizo, hususani mbolea, mbegu na madawa.

Pia waliwashauri wakulima kutumia taasisi za kifedha kama vile Tanzania Agriculture Delelopment Bank (TADB) na National Microfinance Bank (NMB), CRDB, PBZ ili waweze kupata mikopo ya kuendeleza kilimo.







Muonekano wa Kijiji cha mbolea wakati wa maonesho ya nane nane Jijini Mbeya



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo akizungumza na mbunge wa viti maalum Songea Jacqueline Ngonyani Msongozi alipotembelea banda la Mamlaka wakati wa maonesho ya Nanenane Jijini Mbeya.



Mke wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne na mbunge wa jimbo la Mchinga Mkoani Lindi, Salma Kikwete akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kupewa maelezo na Kaimu Meneja wa Kanda ya Mashariki Allan Marik, alipotembelea banda la TFRA wakati wa maonesho ya nanenane Kanda ya Kusini yaliyofanyika katika viwanja vya Ngongo mkoani Lindi kuanzia tarehe Mosi hadi tarehe 8 Agosti, 2023.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. Queen Cuthbert Sendiga (mwenye scarf) akimsikiliza Meneja wa TFRA Kanda ya Kaskazini akieleza majukumu ya Mamlaka alipotembelea banda hilo wakati wa kilele cha maonesho ya sikukuu za wakulima (nane nane) katika viwanja vya Themi-Njiro Mkoani Arusha tarehe 8.8.2023

# Nanenane yaipa wigo TFRA kusambaza elimu ya mbolea

HAKUNA shaka kwamba elimu ya matumizi sahihi ya mbolea katika kilimo sasa imesambaa nchi nzima kwa kuwafikia mamilioni ya walengwa ambao ni Watanzania wa rika zote wanaojishughulisha na sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa taifa.

Ukweli huo umethibitishwa na jitihada za makusudi zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) kuwahamasisha wakulima kuelewa mchango wa pembejeo ya mbolea katika kuongeza tija mashambani ili taifa liweze kujitegemea kwa usalama wa chakula na kuzalisha malighafi kwa mahitaji ya viwanda.

Ni jambo la faraja kwamba TFRA katika miaka ya hivi karibuni imekuwa ikishiriki katika Maenesho ya Nanenane, maonesho yanayofanyika maeneo mbalimbali nchini ili kuwaelimisha wakulima shughuli zake na nafasi ya bidhaa ya mbolea katika kuifanya Tanzania itimize ajenda ya 10/2030 ya kujitosheleza kwa uzalishaji chakula na kuchangia pato la taifa kwa asilimia kumi (10%) kwa mujibu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Mwaka huu 2023 TFRA imekuwa ni chachu ya Maonesho ya Nanenane katika viwanja mbalimbali nchini. Maonesho hayo yalifanyika kitaifa na kimataifa katika Uwanja wa John Mwakangale Jijini Mbeya na katika kanda vituo au kanda nane nchini mwetu.

Kanda hizo ni Nyanda za Juu Kusini katika Jiji la Mbeya, Kanda ya Kati katika jiji la Dodoma, Kanda ya Mashariki Morogoro, Kanda ya Kusini mjini Lindi, Kanda ya Kaskazini ya Mji wa Arusha, Kanda ya Magharibi katika Mji wa historia ya kisiasa wa Tabora, Kanda ya Ziwa kwa mikoa ya Mwanza na Simiyu pamoja na Uwanja wa Amani wa Makolo wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

TFRA ilishiriki maonesho hayo katika viwanja vilivyoainishwa kuanzia Agosti 1, 2023 hadi Agosti 8, 2023, na kuwezesha kuwafikia wananchi kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu majukumu na Sheria iliyoanzisha Mamlaka hiyo, matumizi sahihi ya mbolea, namna serikali itakavyotekeleza mpango wa mbolea za ruzuku kwa mwaka 2023/ 2024, kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu mbolea kwa wadau mbalimbali na kujibu maswali mbalimbali yaliyoulizwa na wananchi waliotembelea mabanda yake.

Mwaka huu wa 2023, TFRA ilishiriki Maonesho ya Nanenane katika kanda tano na viwanja tisa ambavyo ni Themi-Njiro - Kanda ya Kaskazini, John Mwakangale - Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Amani-Makolo wilayani Mbinga mkoani Ruvuma, Nyamhongolo - Kanda ya Ziwa na viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu. Viwanja vingine ni Nzuguni Jijini Dodoma, Uyui mkoani Tabora - Kanda ya Magharibi na viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Morogoro - Kanda ya Mashariki na Ngongo mjini Lindi.

Maonesho haya yalkuwa ni faraja kwa TFRA kwa sababu wananchi wapatao 3,163 walipata fursa ya kutembelea mabanda yake kwa kanda zote kwa uwiano ufuatao: Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - 1,600, Viwanja vya Amani-Makolo - 3,21, viwanja vya Nyamhongolo Kanda ya Ziwa - 461, na viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu - 244. Kwa Kanda ya Kati, wananchi waliotembelea mabanda ni 331, Kanda ya Magharibi (Tabora) - 256, Kanda ya Kaskazini-500 na Kanda ya Pwani - 258. Katika viwanja vya Ngongo mkoani Lindi wananchi 192 walitembelea banda la TFRA.

Katika maeneo yote yaliyotajwa hapo juu TFRA ilijikita kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea pamoja na namna Mamlaka itakavyosimamia utekelezaji wa mpango wa mbolea za ruzuku zilizotolewa kwa wakulima mwaka wa fedha 2022/ 2023 kwa kuwasihi wakulima kujitokeza kujisajili na kuhuisha taarifa zao za usajili ili wanufaike na mpango huo.

Suala la kufurahisha ni kwamba ushiriki wa TFRA katika maonesho ya Nanenane kwa nchi nzima uliambatana na uzinduzi wa bei mpya za ruzuku ya mbolea kwa msimu wa kilimo wa 2023/2024 uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia amekuwa ni mhimili muhimu kitaifa kwa kuhamasisha Watanzania kuimarisha sekta ya kilimo inayoajiri zaidi ya asilimia 75 au 80 ya Watanzania wote wapatao zaidi ya milioni 60, kwa mujibu wa sensa ya mwaka jana 2022.

Amekuwa ni nguzo ya watu wa tabaka la chini wanaoelea katika dimbwi la umaskini ingawa wanajitoa mhanga kwa kutumia nguvu zao kulilisha taifa hili tajiri kwa kila aina ya raslimali.

Katika Maonesho ya 2023, TFRA ilishiriki kwa kuwa moja ya sehemu ya kampuni za mbolea kwa muundo wa Kijiji cha Mbolea ikisambaza kauli mbiu ya Nanenane 2023 ya "Vijana na Wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu ya chakula" kwa kutambua na kuthamini mchango wa vijana na wanawake katika maendeleo kupitia sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Wakale, yaani watu walioishi mamilioni ya miaka kabla yetu, walisema kwamba "Mcheza kwao hutuzwa." Kwa hakika, ni jambo jema kusifu jitihada zinazofanywa na TFRA na taasisi nyingine za serikali kuhubiri injili ya mbolea ili kuwakomboa wakulima wa Tanzania ambao kwa miongo mingi wamekuwa wakiishi katika maisha duni yasiyokuwa na mbele wala nyuma. Mungu ibariki Tanzania!



Mafisa Udhibiti Ubora wa TFRA kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mfugale(kulia) akifuatiwa na Christian Mushoborozi wakitoa elimu ya matumizi sahihi ya bolea kwa wataalam kutoka Idara ya Ardhi na Idara ya Kilimo na Mifugo Halmashauriya Wilaya ya Mbinga wakiwa wameambatana na mgeni Mhe. Alex Nonosius Ngui








Mafisa Udhibiti Ubora wa TFRA kanda ya Nyanda za Juu Kusini Chimile Mfugale(kulia) akifuatiwa na Christian Mushoborozi wakitoa elimu ya matumizi sahihi ya bolea kwa wataalam kutoka Idara ya Ardhi na Idara ya Kilimo na Mifugo Halmashauriya Wilaya ya Mbinga wakiwa wameambatana na mgeni Mhe. Alex Nonosius Ngui



Afisa udhibiti Ubora wa TFRA kanda ya Nyanda za Juu Kusini Henerico Renatus akiitoa elimu ya mbolea kwa wanafunzi wa shule ya wavulana ya Uwata mkoani Mbea walipotembelea banda la Mamlaka katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.

# TFRA ILIVYOJIZOLEA TUZO KWA UTENDAJI ULIOTUKUKA



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Michael Sanga Akipokea cheti cha mshindi wa pili katika kundi la taasisi za udhibiti zilizoshiriki maonesho ya nanenane jijini Mbeya.

Kama wahenga walivyosema: "Mcheza kwao hutuzwa." Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa TFRA baada ya kuzoa tuzo mbaLimbali kwa utendaji uliotukuka. Katika Maonesho na sherehe za wakulima (nanenane) mwaka huu 2023, TFRA ilishindanishwa na taasisi nyingine za udhibiti katika umahiri kulingana na vigezo vilivyowekwa na Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Nanenane. Kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, TFRA ilifanikiwa kushika Nafasi ya Pili katika kundi hilo na kutunukiwa cheti.

Katika Kanda ya Ziwa kwenye maonesho yaliyofanyika viwanja vya Nyamuhongolo mkoani Mwanza, TFRA ilitunukiwa tuzo za Mshindi wa Pili na Mshindi wa Tatu kwa Maonesho yaliyofanyika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Kwa ujumla, kwa kanda zote, mabanda ya TFRA yalikuwa ni kivutio kwa wageni waliohusika kufungua na kufunga maonesho kama vile huko Arusha, Dodoma na Tabora.

Ni dhahiri kwamba TFRA ilipata nafasi adhimu ya kutangaza shughuli zake kwa wadau wa kilimo na taasisi nyingine zisizo za serikali.

Ni kwa mantiki hiyo tunaweza kusema kwamba injili ya mbolea iliwafikia watanzania wengi kuhusu ubora wa mbolea na matumizi sahihi katika kilimo.

Jambo jingine la msingi ni kwamba elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa mpango wa mbolea za ruzuku kwa msimu ujao wa kilimo 2023/2024 iliwafikia wakulima wengi angalau kwa nchi nzima kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo.

Elimu kwa umma si jambo la kufanyiwa papara; ni jambo linalohitaji mwendo wa polepole kuwafanya wananchi waelewe mikakati ya maendeleo ya taifa lao. Hivyo ndivyo TFRA inavyofanya kuwakusanya wakulima kwa vitendo na kuwaelimisha kuhusu matumizi sahihi ya mbolea ili waondokane na umaskini kwa kuongeza tija mashambani.

Kwa hakika, tunaweza kutabiri kwamba kwa miaka ijayo Tanzania itakuwa kapu la chakula barani Afrika ikiwa mikakati iliyobuniwa sasa na serikali itazaa matunda kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wake. Kujitegemea kwa chakula na kufikia lengo la kilimo biashara ni lazima Watanzania wafanye kazi kwa bidii.

Hivi sasa wajuzi wa mambo tayari wameshaonya kwamba tatizo la njaa linazidi kuongezeka duniani na kuna hatari kuwa iwapo hatua za makusudi hazitachukuliwa kukabili tatizo hilo, watu wengi huenda wakafa kutokana na janga hilo.

Hili ni somo ambalo Watanzania ni lazima walielewe kwa mawanda mapama ili kuepuka janga hili la njaa inayotishia dunia. Ni lazima kila Mtanzania mahali alipo atimize wajibu wake kama alivyowahi kusema mwasisi wa taifa hili miaka ya mwanzo wa uhuru.

# HABARI KATIKA PICHA



Watumishi wa TFRA walioshiriki maonesho na sherehe za wakulima katika viwanja vya Amani Makolo wilayani Mbinga wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kutunukiwa cheti cha ushiriki katika maonesho hao



Watumishi wa TFRA walioshiriki maonesho ya nanenane Kanda ya Kati Dodoma wakifurahia cheti cha ushiriki mara baada kuhitimisha sherehe na aonesho ya wakulima yaliyofanyika kuanzia tarehe 1 hadi 8, 2023



Watumishi wa TFRA wakifurahia kombe la Mshindi wa pili katika maonesho yaliyofanyika viwanja vya Nyamuhongolo mkoani Mwanza.



Watumishi wa TFRA wakifurahia tuzo ya Mshindi wa tatu viwanja vya Nyakabindi kanda ya Ziwa Magharibi mara baada ya sherehe na sikukuu ya wakulima kufikia kilele chake tarehe 08.08.2023



Watumishi wa TFRA wakimsikiliza kwa makini mkulima aliyetembelea banda la mamlaka wakati wa maonesho yaliyokuwa yakiendelea katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu


MAMA QUENE UMEFIKA BANDA LA TFRA?
HAPANA! KUNA NINI?
NENDA NDUGU YANGU, NILISIKIA UNALALAMIKA, UMETUMIA MBOLEA LAKINI MAZAO YAMEGOMA. UKIFIKA PALE WATAKUELEKEZA NJIA SAHIHI YA KUTUMIA MBOLEA ILI KUONGEZA TIJA KWENYE KILIMO, TENA WANASEMA SI KILA ARDHI INAHITAJI KUTUMIA DAP, CAN AU UREA NI HADI UJIRIDHISHE KWA KUPIMA AFYA YA UDONGO WA SHAMBA LAKO NDIPO UTAJUA MBOLEA UNAYOTAKIWA KUWEKA NA HIVYO KUONGEZA TIJA!
EEH! HII SI YA KUKOSA UKIZINGATIA MWAKA HUU NIMETUMIA GHARAMA KUNUNUA MBOLEA NA SIJAVUNA KAMA NILIVYOTARAJIA, NGOJA NIENDE!
NI MUHIMU SANA, MWENZIO NIMEWAPIGIA SIMU NA NDUGU ZANGU WA LINDI WATEMBELEE BANDA LA TFRA
KWANI TFRA WANASHIRIKI MAONESHO NA MIKOA MINGINE? NILIJUA NI MBEYA TU
HAPANA! WAPO KANDA ZOTE NCHINI KAMA UNA NDUGU LINDI, MBINGA, MWANZA,SIMIYU MOROGORO, WAAMBIE WATEMBELEE BANDA LA TFRA
SAWA SAWA!

# HABARI KATIKA PICHA









Watumishi wa TFRA wakifurahi ndani ya banda la Mamlaka siku ya kilele cha maadhimisho ya sikukuu za wakulima katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya

# Wakulima wa Makambako wanufaika na elimu ya mbolea nanenane

Wakulima wapatao hamsini (50) kutoka Makambako Mji wamenufaika na elimu ya matumizi sahihi ya mbolea mara baada ya kutembelea banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) katika maonesho ya nanenene yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.

Akizungumza na wakulima tarehe 6 Agosti, 2023 bandani hapo, Afisa Udhibiti Ubora wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Henerico Renatus aliwataka wakulima kutumia mbolea mara baada ya kupima afya ya udongo na kubaini aina ya virutubisho vinavyohitajika katika udongo huo.

Alisema, kutumia mbolea kwa mazoea kunapelekea kuweka mbolea isiyohitajika kwenye udongo huo na kusababisha mkulima kupoteza pesa kutokana na aina ya mbolea iliyotumika kutokuongeza tija kwenye zao husika.

Akizungumza kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, Heneriko alieleza kuwa, kuna kanuni nne za matumizi sahihi ya mbolea ikiwa ni kutumia mbolea sahihi kwa kiwango sahihi, wakati sahihi na sehemu sahihi.

Akifafanua kuhusu kanuni za matumizi sahihi ya mbolea, Heneriko alisema kila zao lina mahitaji yake ya mbolea ambayo hutofautiana kulingana na zao husika na kuwataka wakulima kuchagua mbolea sahihi kulingana na virutubisho vilivyopo kwenye mbolea husika na mahitaji ya zao husika pamoja na afya ya udongo ilivyo.

Akielezea kuhusu kiwango cha mbolea kinachopaswa kutumika kulingana na zao, Henerico alieleza kuwa, lazima mkulima azingatie hali ya udongo na mahitaji ya zao kabla ya kuweka mbolea na kwa upande wa sehemu sahihi ya kuweka mbolea alieleza kuwa, mkulima anatakiwa kuweka mbolea mahala ambako mizizi inaweza kufika na kufyonza virutubisho hivyo.

Aidha, Henerico aliwaeleza wakulima kuhusu namna virutubisho vinavyopotea kwenye udogo na kueleza kuwa njia ya kwanza inayosababisha virutubisho kupotea kwenye udongo ni kuchujika ambapo virutubisho kwenye mbolea za madini huyeyuka na kunyonywa kwa urahisi na mmea pia huchujika kwenda chini zaidi ya mizizi hususan kirutubisho cha nitrojeni.

Akieleza njia nyingine ya kupotea kwa virutubisho kwenye udongo alisema ni njia ya mvuke na kuhama kwa virutubisho (Run off) kunakoweza kutokea wakati wa mvua kubwa au mafuriko.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima kutoka Makambako, mkulima Burton Sadaka Sanga wa tawi la Azimio Kata ya Mwembetogwa alisema amenufaika na elimu inayomtaka kuhakikisha anapima afya ya udongo kabla ya kutumia mbolea katika shamba lake, aidha kutokutumia mbolea wakati wa mvua ama jua kali na kuelezwa kuwa, wakati mzuri anaopaswa kutumia mbolea ni wakati udongo unapokuwa na unyevunyevu.

Sanga aliahidi kutumia elimu aliyoipata katika kuwaelimisha wakulima wengine ambao hawakupata nafasi ya kuhudhuria kwenye maonesho ya nane nane mwaka huu ili na wao waweze kuongeza tija kwenye kilimo chao.

Naye mkulima Cleopa Lufumbe aliishukuru serikali kwa kuwakumbuka wakulima na kutoa mbolea za ruzuku zilizosaidia kuongeza tija katika kilimo chao na kuwataka wakulima kuhakikisha wanapima afya ya udongo kabla ya kutumia mbolea.



Afisa Udhibiti Ubora wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Henerico Renatus (mwenye t-Shirt ya kijani) akitoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima kutoka mjini Makambako walipotembelea banda la Mamlaka wakati wa maonesho ya nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya tarehe 06 Agosti, 2023.

# HABARI KATIKA PICHA





Wananchi kutoka mjini Makambako wakifuatilia elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kutoka kwa wataalamu wa TFRA walipotembelea banda la Mamlaka tarehe 6 Agosti, 2023









# TFRA yaombwa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima

Mwenyekiti wa halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Donald Mejetii ameiomba Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakazi wa Dodoma kutokana na kuwa na hofu ya kutumia mbolea kwenye shughuli mbalimbali za kilimo.

Mejetii ambaye alikuwa mgeni rasmi,alitoa ombi hilo tarehe 8 Agosti, 2023 Jijini Dodoma alipotembea banda la Mamlaka wakati wa maonyesho ya wakulima Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma kwa Kanda ya Kati.

Alisema Dodoma ni kame hivyo wakulima wengi hutumia mbolea bila maelekezo ya kitaalam na kupelekea mazao kukauka kutokana na kutokujua matumizi sahihi ya mbolea.

“Naomba TFRA muweke jitihada za kutoa elimu kwa wakazi wa Dodoma, tunahitaji kutumia mbolea,”Alisema Mejetii.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati, Joshua Ng’ondya alisema wakazi wa Dodoma wanapaswa kutumia mbolea pindi msimu wa mvua unapoaanza ili iweze kukutana na unyevu.

Alisema mbolea inapowekwa shambani kunatakiwa kuwa na unyevunyevu hivyo mikoa ambayo ni mikame inapaswa kuweka mbolea ya kupandia pindi tu mvua inaponyesha.

“Tutaendelea kutoa elimu kwa wakazi Dodoma juu matumizi sahihi ya mbolea pamoja na umuhimu wake,”Alikazia Meneja Ng’ondya.








# WAKULIMA WAISHUKURU TFRA UTEKELEZAJI MPANGO WA MBOLEA ZA RUZUKU

WAKULIMA wameishukuru Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kubuni mbinu ya kutoa namba ya siri itakayowawezesha mkulima kupata mbolea ya ruzuku bila tstizo lolote.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika maonyesho ya Kanda ya Kati ya wakulima Nane Nane yanayoendelea katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma,Mkulima Ibrahim Ndondole amesema kitendo cha mkulima kupewa namba kitasaidia wakulima kupata kwa urahisi mbolea ya ruzuku.

“Tunawashkuru sana TFRA kwa kubuni mbinu ya kutoa namba ya siri itakayomuwezesha Mkulima kupata mbolea ya Ruzuku,tunaomba waendelee kubuni mbinu mbalimbali ili kuhakikisha uchakuaji wa mbolea unatoweka,”Amesema Ndondole.

Mbali na hilo wameipongeza mamlaka hiyo kw kuboresha mfumo wa utoaji mbolea ya ruzuku tofauti na ilivyokuwa awali, wakulima wengi walipata changamoto ya kujisajili ikiwemo kupata mbolea ya ruzuku.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati Joshua Ng’ondya amesema hivi sasa Mamlaka hiyo imeweka mikakati ya kutumia vyama vya ushirika ili kupata mawakala ambao watafanya kazi kwa weredi.

Mbali na hilo alisema wametoa elimu kwa mawakala zaidi ya 150 ambao watakwenda kufanya kazi ya usambazaji mbolea ya ruzuku kwa wakulima mbalimbali hapa nchini.

Kutokana na hilo amesema msimu huu hakutakuwa na malalamiko yoyote ya kukosa mbolea ya ruzuku kutoka kwa wakulima

Hata hivyo amesema msimu huu TFRA imejipanga kuhakikisha hakuna malalamiko yoyote ya uchakajuaji mbolea huku akisisitiza atakayebainika anafanya vitendo hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.










**TFRA ›› NANENANE DODOMA**

Afisa Udhibiti Ubora kutoka Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania-TFRA Gema Nganyagwa (wa kwanza kushoto) Akitoa Elimu ya Matumizi sahihi ya Mbolea kwa Lugha ya Alama Kwa Mwenyekiti wa Kikundi Cha Watu Wenye Ulemavu wa Kusikia Mkoani Dodoma.






# Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika: Nafasi pekee kuwavuta wawekezaji Tanzania

Tanzania imebeba matumaini makubwa kwamba Mkutano wa 13 wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika utakaofanyika Dar es Salaam kuanzia Septemba 5 hadi 8 utaleta neema na kuwa kichocheo cha kuwavuta wawekezaji wakubwa katika sekta muhimu ya kilimo kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Mkutano huo, unaotarajiwa kuhudhuria na washiriki wapatao 3,000, utajadili kwa kina mikakati ya kivitendo na njia sahihi za kulifanya bara la Afrika lijitegemee kwa usalama wa chakula.

Wadau wa Jukwaa hilo watatoka katika makundi ya wataalam, watafiti, watunga sera,wanasiasa na wakulima wadogowadogo. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Kilimo iliyotolewa na Katibu Mkuu, Gerald Mweli, baadhi ya marais wa Afrika wameonyesha nia ya kushiriki katika mkutano huo wakimuunga mkono mwenyeji wao, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Baadhi ya wazungumzaji wakuu ni pamoja na Rais Dkt. Samia, Waziri Mkuu wa zamani wa Ethiopia Hailemariam Dessalegn, Waziri wa Kilimo wa Tanzania, Hussein Mohamed Bashe, na viongozi wengine mashuhuri kutoka ndani na nje ya nchi.

Mkutano huo utakaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Julius Nyerere, pia utajikita katika kuzungumzia masuala ya ubunifu, teknolojia na jinsi ya kulikwamua bara la Afrika dhidi ya janga la njaa ambalo wataalam wanaonya huenda likaikumba dunia kwa miaka ya usoni.

Viongozi wa Tanzania, akiwemo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wanauona mkutano wa Dar es Salaam kama fursa ya pekee kwa taifa hili tajiri kwa rasilimali ya kuuvuta ulimwengu kuja kujionea yale yaliyotendeka na yatakayotendeka katika kuligeuza bara la Afrika kuwa ghala la dunia kwa usalama wa chakula.

“Kwa serkali ya Tanzania, mkutano huu wa kimataifa ni nafasi pekee ya kuimarisha uhusiano na ubia utakaosukuma mipango yetu ya kubadili mifumo yetu ya chakula, “ anaeleza Waziri wa Kilimo , Hussein Bashe.

“Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu, ambao mchango wake kwa pato la taifa ni sawa na theluthi moja kama ilivyo katika nchi nyingi za Afrika.

“Jukwaa la Mifumo ya Chakula 2023 linalotarajiwa kuzua mijadala mizito kuhusu masuala ya fedha duniani, hasa katika kukidhi changamoto zinazolikabili bara la Afrika linapokuja suala la usalama wa chakula, yatajadiliwa kwa kina, “ Waziri Bashe anasema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo, anaipongeza serikali kwa kuandaa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika 2023 kwamba utaifanya nchi itambulike kote duniani , hasa kwa washiriki ambao watakuwa ni mara yao ya kwanza kukanyaga ardhi ya taifa lililojaliwa kwa raslimali za kila aina.

“Watu 3,000 wanaotarajiwa kuhudhuria mkutano watambeba ulimwengu kuuleta Tanzania na kuibeba Tanzania na kuipeleka ulimwenguni. Jukwaa litakuwa fursa kwa Tanzania kujitwalia soko la chakula kinachozalishwa nchini mwetu,” anasema Dkt. Ngailo.

“Mkutano huu una manufaa kwa chi yetu kwa sababu Tanzania ina mchango mkubwa kuhusu upatikanaji wa mbolea ambayo ni pembejeo muhimu kwa uzalishaji wa chakula. Kwetu sisi TFRA itakuwa ni fursa ya kueneza injili ya umuhimu wa mbolea katika kukuza uzalishaji katika kilimo,” anaongeza.

Mchumi mwandamizi wa TFRA, Elizabeth Bole, ambaye pia ni Kaimu Meneja wa

# Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika: Nafasi pekee kuwavuta wawekezaji Tanzania

Ununuzi Mbolea wa Pamoja, yeye anasema kuwa atakuwa makini katika mkutno huo wakati majadiliano kuhusu mchango wa mboea katika kilimo. "Mchango wa mbolea katika kilimo ni suala ambalo halihitaji mjadala mrefu kwa kuwa uchumi wa Tanzana na nchi nyingine za Afrika unategemea sana kilimo. Ili uchumi ukue kwa kasi ni lazima kuwe na matumizi sahihi ya mbolea.

Katika harakati za kuimarisha kilimo, serikali ya Tanzania mwaka jana ilitenga shilingi bilioni 150 kama ruzuku ya mbolea kwa wakulima kuwasaidia waongeze uzalishaji na kupunguza makali ya bei ya bidhaa hiyo katika soko la dunia, hasa baada ya kuzuka kwa vita kati ya Urusi na Ukraine.

Kwa mujibu wa Dkt. Ngailo, katika siku za usoni Tanzania itakuwa kitovu cha mbolea barani Afrika kama mikakati ya sasa iliyobuniwa na serikali ya kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya mbolea itakwenda kama ilivyopangwa.

Hivi sasa Tanzania inashuhudia kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea ili kukidhi mahitaji makubwa ya bidhaa hiyo katika sekta ya kilimo. Nia ya kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea ni kuwapunguzia wakulima bei ili mbolea ipatikane kwa urahisi kwa kuwafikia wakulima hao mahali walipo.

Lengo jingine la kuwavuta wawekezaji katika ujenzi wa viwanda ni kuwa na soko linaloaminika la bidhaa hiyo kwa nchi jirani za Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika pamoja na mataifa mengine ya Ulaya ambayo yamekuwa yakiiagiza mbolea kutoka kiwanda cha Minjingu mkoani Manyara.

Mahitaji ya mbolea kwa wakulima wa Tanzania katika miaka ya karibuni yameongezeka kutoka tani 42,000 mpaka tani165,000 baada ya kuwepo kwa jitihada za kuwaelimisha wakulima kutumia mbolea ili waongeze tija katika mashamba yao, kwamujibu wa Bole.

Ni faraja kwamba ongezeko la matumizi ya mbolea limezaa matunda baada ya kushuhudia ongezeko la uzalishaji wa chakula kutoka tani milioni 17 hadi kufikia tani milioni 20, anaeleza Dkt. Ngailo.

"Kazi ya kuwaelimisha wakulima kutumia mbolea ni suala endelevu kwa kushirikiana na serikali za mitaa. Kuna uwezekano mkubwa kwa wakulima wengi Tanzania kutumia mbolea na hatimaye kulilisha bara la Afrika," anaeleza Dkt. Ngailo.

"Ruzuku ya mbolea imesaidia sana wakulima kununua mbolea kwa wingi ikilinganishwa na miaka ya nyuma.'

Dkt. Ngailo anaeleza kuwa ongezeko la matumizi ya mbolea miongoni mwa wakulima limewapa viongozi ari ya kujiamini kwamba Tanzania katika miaka michache ijayo itafikia lengo lake la kulisha bara zima la Afrika kutokana na ziada ya chakula kinachozalishwa.

"Inawezekana kwa Tanzania kulisha Afrika na dunia nzima. Tuna uwezo wa kuzalisha chakula cha ziada kukidhi mahitaji ya Afrika na dunia nzima," anasema kwa kujiamini , huku akiungwa mkono na mchumi mwandamizi wa TFRA, Elizabethi Bole.

Kwa dhamira ya Tanzania kujitosheleza kwa chakula na kuwa ghala la kuaminika kwa Afrika na dunia nzima, mkutano wa 13 wa Jukwaa la Chakula Afrika 2023 utakuwa na mambo mengi ya kujionea ambayo yatafaa yaigwe na mataifa mengine kuwa fundisho.

Kama alivyosema Dkt. Stephan Ngailo, dunia itakuja Tanzania kushuhudia yaliyopo na itaondoka na mafunzo kwenda kuyapandikiza sehemu nyingine; na hivyo kuliuza jina la Tanzania ughaibuni.